JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Januari, 2026**
Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MOSHI**

**Namba za Simu**
Mkuu wa Shule ……….0763318438
Makamu Mkuu wa Shule ..0765008077
Matron …………………0753934593
Patron …………………0629900277
Shule ya Sekondari ya Ufundi Moshi
S.L.P 3014 **MOSHI**
Tarehe 20.11.2025



CamScanner

# HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI.
# SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MOSHI.

S.L.P 3014, Simu 0755 011 478, Tovuti: https://moshitechnical.weebly.com/ Barua pepe: moshitechnical63@gmail.com Instagaram: moshitech

Bandika Picha Hapa

Admission Na ____________(Inapatikana shuleni)

**Jina la Mwanafunzi** (*Kama yanavyoonekana kwenye matokeo ya darasa la saba*):

Jinsi: (*Weka ✓panapohusika*) **ME** **KE**

S.L.P ________________________________________

________________________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MOSHI ILIYOKO MANISPAA YA MOSHI MKOA WA KILIMANJARO (JOINING INSTRUCTION)**

1. Tunafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza **Mwaka 2026** hapa Shule ya Sekondari Ufundi Moshi. Shule hii ni ya bweni na ina mchanganyiko wa wavulana na wasichana.Shule ipo kilometa tano kutoka Moshi Mjini kando ya barabara Kuu ya Moshi-Arusha.

Usafiri wa magari madogo hiace/daladala unapatikana kwa nauli ya Tsh **700/=** na kwa taxi ni wastani wa Tsh **5000/=.** Bajaji ya kukodi ni Tsh **4000/=**

Wewe ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliobahatika kuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari hivyo unatakiwa kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza maagizo yote kwa Busara, Hekima, Utii na Uaminifu. Shule itafunguliwa tarehe **13.01.2026** na unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe **12.01.2026** kabla ya saa kumi na mbili jioni.

Unatakiwa kugharamia safari ya kuja shuleni na pia uhakikishe una nauli ya kurudi nyumbani wakati shule itakapofungwa mwishoni mwa kila muhula.

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**A. SARE YA SHULE:**

Mzazi anatakiwa kumnunulia mwanae sare ya shule kama ifuatavyo:

**(i) WASICHANA;**

1.Sketi mbili za **rangi ya Khaki (Na.1023/khaki ya polisi)**. Sketi ziwe na Marinda 16 (nane kila upande) yaliyopangwa kuelekea kulia na ziwe ndefu zinazofika kwenye vifundo vya miguu.

2.Shati mbili nyeupe aina ya tomato za mikono mifupi

3.Tai ya rangi kama ya sketi



CamScanner

**Kwa wanafunzi wasichana wa Kiislamu wanapaswa kuwa na: -**

4. Sketi 2 za **rangi ya Khaki (Na.1023/khaki ya polisi)** ndefu zinazofika katika vifundo vya miguu, zenye marinda tajwa hapo juu.

5. Ushungi 2 nyeupe ziwe pana, ndefu na zinazositiri vizuri. Ushungi **haupaswi** kufunika viganja vya mikono, isifunike uso pia isiwe nyepesi na wala isiwe na urembo wowote.

6. Blauzi (Nusu Kanzu) 2 nyeupe za mikono mirefu zisizofunika viganja vya mikono, ziwe pana zisibane, pia ziwe ndefu zinayoishia juu ya magoti, isiwe kama gauni na isiwe nyepesi.

**(ii) WAVULANA;**

1. Suruali **2** za **rangi ya Khaki (Na.1023/khaki ya polisi)**. **zisiwe za kubana** (*vibamba*) na ziwe na **marinda mawili** na upana wa inchi 18 miguuni
2. Mkanda mweusi usiwe mpana sana wala usiwe na bakoli/chata kubwa ya kubandika. (Pia hupatikana shuleni kwenye idara ya Ngozi kwa bei nafuu)
3. Shati mbili nyeupe aina ya tomato za mikono mifupi
4. Tai ya rangi kama ya suruali

**Mahitaji ya Pamoja**

1. Madaftari 14 makubwa (Counter books) Quire 3 au Zaidi.
2. Begi la kubebea madaftari (SCHOOL BAG) Liwe na mikanda ya kuvaa mgongoni. Lisiwe la plastiki/nailoni wala lenye maandishi makubwa au picha.
3. Kompasi (Mathematical set).
4. Kalamu, Penseli, rula, vifutio vya kutosha.
5. KAMUSI (English/Swahili) **kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kamusi yake.**
6. Rim 2 za karatasi nyeupe **A4** kwa ajili ya kuchapishia mitihani na Rim 1 ya karatasi zenye mistari (***rulled papers***) kwa ajili ya kujibia mitihani, Rim 1 ya A3 kwa ajili ya michoro na karatasi za grafu (graph papers) 1
7. Fagio la chelewa lenye mpini mrefu (wote)
8. Sabuni ya maji lita 5 (Zingatia ubora. Mf. Dexi n.k)
9. Squizer (Mopper)
10. Jembe 1 lenye mpini
11. Panga 1 (Wavulana) .Fyekeo 1 (Wasichana)
12. Fagio 1 la kufuta buibui *(wasichana)*
13. 'Soft broom' (Wavulana)
14. 'Hard broom' (Wote)
15. '**Ovaroli'** moja la rangi ya kahawia. Liwe na mifuko mikubwa
16. Pazia spesho pea moja za Rangi ya pink (Wasichana tu)
17. Soksi nyeupe jozi 4 au zaidi
18. Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visivyokuwa na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Lazima viwe vya kufunga kwa kamba (Pia hupatikana kwenye kiwanda cha Ngozi kilichopo Jirani na shule)
19. Sweta 1 au zaidi la mikono mirefu ya rangi ya rangi ya Khaki lenye shingo ya V.
20. Track suti ya rangi ya **njano** na Tisheti ya **rangi ya njano** (yenye kola) itakayopigwa nembo ya shule ambayo utaruhusiwa kuivaa ndani na nje ya shule (Pia inapatikana kwenye maduka ya shule kwa gharama ya Tsh. **15,000/=)**
21. Malapa kwa ajili ya kuogea (Sio yeboyebo)
22. Sandles za rangi nyeusi kwa ajili ya kushindia nje ya Darasa.



CamScanner

23. Saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda (yenye alarm)
24. Kikokotoo (Calculator) casio yenye f(x) 991,
25. PPE(Personal Protective Equipments) ambazo ni Safety boots, Kofia ngumu, Gloves ngumu, Dust mask na Miwani ngumu na Reflector ya rangi ya njano kwa sababu wote watasoma masomo ya AMALI

**N.B: Baadhi ya vifaa kama vile, madaftari, kompasi,vifaa vya usafi,Rim na godoro vinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule.**

**B. MAVAZI YA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) NA MICHEZO;**

**(i) WASICHANA;**

1. Sketi 2 nyeusi ziwe na marinda 16 (nane kila upande) yaliyopangwa kuelekea kulia na ziwe ndefu za kufunika vifundo vya miguu.
2. Kwa wasichana wa kiislamu, hijab zinapaswa kuwa na rangi nyeusi zinazofunika kifua na zisiwe na urembo wowote.
3. Tisheti 2 (shamba dress) **rangi ya kahawia (yenye kola)** na zisiwe na maandishi au chata yoyote.

**(ii) WAVULANA;**

1. Suruali 2 nyeusi zenye marinda mawili, iwe ndefu na isiwe ya kubana (Kibamba)
2. Tisheti 2 (shamba dress) **rangi ya kahawia** na zisiwe na maandishi au chata yoyote.

**(iii) NGUO ZA MICHEZO KWA WAVULANA NA WASICHANA:**

26. Raba (njumu), bukta na T-shirt zenye **rangi ya njano** na zisiwe na maandishi au chata yoyote. Epuka kuleta jezi za timu yoyote.

**NB; Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za aina nyingine tofauti na zilizotajwa hapo juu,pia perfume za aina yoyote haziruhusiwi. Akikutwa nazo atawajibishwa.**

## C. MAHITAJI MENGINE:

1. Gododro la Sponji Lenye Ukubwa Wa Futi 2½X6.
2. Shuka 2 za rangi ya bluu bahari (light blue). kwa wavulana na rangi ya pink kwa wasichana.
3. Mto na foronya 2 za rangi inayofanana na shuka
4. Chandarua kwa ajili ya kuzuia mbu.
5. Blanketi moja
6. Bakuli, sahani, kikombe na kijiko (**Visiwe vya plastic**)
7. Ndoo mbili za maji kwa ajili ya kuogea na matumizi mengine.
8. Sanduku moja imara la bati la kuhifadhia vitu vyako (Tranka lenye kufuli mbili)
9. Vifaa kwa ajili ya usafi wa mwili (dawa ya meno, sabuni ya kuogea, mswaki, rangi ya viatu, brashi, taulo n.k).
10. Nguo za ndani za kutosha.
11. Taulo maalumu **(Pedi)** kwa wasichana.
12. Picha 2- passport size iliyopigwa hivi karibuni (Kwa Shati Jeupe).

## D. VIAMBATISHO VYA KUREJESHA SHULENI.

Mwanafunzi anatakiwa akamilishe/ajaze fomu zifuatazo ambazo baadhi zimeambatanishwa.

1. Fomu ya kupimwa afya. (Medical Examination form). Iwe imejazwa na Daktari wa ngazi ya Wilaya au zaidi (sio Zahanati ) na iwe ni Hospitali ya serikali.
2. Nakala (photocopy) ya cheti cha kuzaliwa
3. Fomu ya taarifa binafsi. (ijazwe na mzazi/mlezi)



CS CamScanner

4. Fomu ya kukubali kutii Sheria za shule. **"mwanafunzi ahakikishe amezisoma kwa makini na kuzielewa akiwa na mzazi/mlezi wake.Zijadiliwe kea kina"**
5. Fomu yenye majina, namba za simu na picha (passport size) za wazazi/ ndugu au jamaa wa karibu wanaoweza kumtembelea au kuitwa shuleni panapotokea tatizo (ziwe zimebandikwa)
6. Uje na hii 'Joining Instruction' ikiwa na kurasa zote ukiwa umekamilisha vitu vyote ikiwa ni pamoja na kujaza kwa usahihi fomu zilizoambatishwa.

**E. BIMA YA AFYA**

Kila mwanafunzi aje na **BIMA YA AFYA** itakayomwezesha kupata huduma mahali popote au fedha kiasi cha Tsh.50,400/ itakayolipiwa kwenye akaunti tajwa hapo juu ili kukata Bima ya pamoja (Hii ni muhimu sana)

**MUHIMU.**

- Wazazi/walezi na ndugu wengine wanaweza kumtembelea mwanafunzi **Jumapili ya Kwanza ya Mwezi Kuanzia Saa Nne Asubuhi Hadi Saa Kumi Jioni**.Mgeni yeyote hataruhusiwa kwenda maeneo ya mabweni wala kumletea **vyakula** mwanafunzi.
- Kukiwa na dharura ambayo inamlazimu mzazi/mlezi aje shuleni siku tofauti, dharura hiyo itashughulikiwa na ofisi ya mkuu wa shule.
- Endapo itatokea tatizo la msiba, mwanafunzi ataruhusiwa kuhudhuria mazishi ya Baba Mzazi, Mama Mzazi, Kaka au Dada wa kuzaliwa pamoja tu.
- Mwanafunzi atapokelewa shuleni akiwa amevaa sare za shule na si vinginevyo. (haruhusiwi kuja akiwa amevaa nguo za nyumbani.
- Shule hii ni ya Serikali, haina Dini maalum na inazingatia katiba na sheria za nchi kuhusu uhuru wa kuabudu. Wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na Imani zao kwa kufuata utaratibu uliowekwa na shule. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba nyingine za shule. Tofauti na hapo mzazi /Mlezi anashauriwa kumtafutia mwanae shule inayoendeshwa kwa misingi ya dini.Mwanafunzi haruhusiwi kubadilisha dini hapa shuleni bila ridhaa ya mzazi
- Mwanafunzi aje na fedha ya matumizi (pocket money) ambayo itatunzwa **kwa mhasibu wa shule** na kupewa kidogo kwa kusaini kadri atakavyokuwa anahitaji. Mzazi/Mlezi anaweza kumtumia mwanae fedha kwa njia ya M PESA kwa kutumia namba ya shule **0755011478** yenye jina **Moshi Technical**. Aidha kabla au mara baada ya kutuma, mzazi /mlezi atatakiwa kutuma ujumbe wa simu (meseji) kutoa taarifa akitaja jina na kidato cha mwanae anayemtumia fedha na kiasi cha fedha alichotuma. **Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na fedha Zaidi ya Tsh.5,000 Bwenini.**

4. **KIKAO CHA WAZAZI**

Kutakua na kikao cha wazazi kitakachofanyika tarehe **22/01/2026** Kuanzia **Saa Tatu Asubuhi**. Lengo la vikao hivyo ni kumpa mzazi fursa kuona shule ya mwanae anayosoma na kujua mipango na maendeleo ya shule hususan jinsi ya kukuza taaluma na nidhamu ya wanafunzi. Uongozi wa shule unategemea pia michango ya mawazo ya wazazi jinsi ya kutatua changamoto zilizopo shuleni ili kuifanya iwe bora Zaidi.Hii fursa ni adhimu sana kwa sababu hufanyika mara moja tu kwa mwaka. Tafadhali mzazi jiandae kwa vikao hivyo.

5. **TAHADHARI:**

Tunza fedha na vifaa vyako uwapo safarini. Epuka kupokea vyakula kutoka kwa mtu usiyemfahamu.

**Pia ni marufuku kumpatia mwanao simu awapo shuleni**

Nakutakia Safari njema na karibu sana.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MOSHI**

**P. S. MWANGA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
MOSHI TECHNICAL SEC. SCHOOL
P. O. Box 3014
MOSHI

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

Sheria, kanuni, na taratibu za Shule zimewekwa kwa lengo la kumwezesha mwanafunzi kuelimika na kumaliza elimu yake kwa utulivu na mafanikio makubwa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayevunja sheria, kanuni na taratibu hizo kwa makusudi. Hatua hizo ni pamoja adhabu ndogondogo shuleni, kusimamishwa shule na au kufukuzwa shule kulingana na uzito wa kosa. Hivyo ni vyema kila mwanafunzi afuate sheria, kanuni na taratibu hizo kwa kutumia hekima, akili, bidii, utii busara na uaminifu ili kuepukana na uvunjifu wa sheria, kanuni, na taratibu za shule usiokuwa wa lazima.

### 1. HESHIMA, USAFI NA UTUNZAJI WA MALI YA UMMA.

**Kila mwanafunzi anatakiwa**

(i) Kuheshimu Walimu na wafanyakazi wasio walimu, Wanafunzi wenzake na wanajumuiya wote.

(ii) Kushiriki kwa bidi sana katika kazi mbalimbali za Shule.

(iii) Kuheshimu ratiba nzima ya Shule bila kukosa kusanyiko lolote,vipindi vya Dini,*Preparation* zote n.k

(iv) Kila mwanafunzi atapangiwa eneo lake la kufanyia usafi kila siku na pia atakuwa na zamu ya kudeki darasa, bwalo la chakula, vyoo, na bweni lake na atatakiwa kufanya usafi kwa wakati uliopangwa.

(v) Kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule wakati wote anapotakiwa na awe tayari kwa ukaguzi wakati wowote.

(vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zote zilizopo shuleni. Mwanafunzi atakaye haribu au kupoteza mali ya shule kwa makusudi au uzembe atawajibika kulipia uharibifu au upotevu huo.

(vii) Mwanafunzi anapaswa kuoga kwa brashi aliyoizoea (Aje nayo) angalau mara moja kwa masaa 24. Kwa mwenye changamoto za kiafya taarifa zake zitolewe kwa daktari ili apewe huduma stahiki

(viii) Ni marufuku kupeleka chakula bwenini kwa ajili ya usalama wako na shule kwa ujumla

**NB: Atakayekiuka maelekezo haya atakabiliwa na adhabu zilizoainishwa na Serikali ya wanafunzi na kupitishwa kwenye baraza la shule.**

**Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kufanya yafuatayo: -**

(a) Kuvuta sigara, bangi wala madawa ya kulevya

(b) Kufuga kucha, nywele wala ndevu

(c) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima kama sketi fupi au suruali ya kubana

(d) Kugombana, Kutukana au kutoa lugha za matusi kwa mtu yeyote

(e) Kunyoa nywele, mitindo ya kihuni kwa mfano kipara, panki/kiduku au kusuka

(f) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule

(g) Kubeti,kucheza PS,kamari n.k

(h) Kupaka kucha rangi au kutia nywele dawa

(i) Kupaka lipstick au kutinda nyusi na kupaka wanja.

### 2. MAHUDHURIO.

**(i)** Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria:

**(ii)** Vipindi vyote vya masomo ya darasani na vya nje ya darasa.

**(iii)** Miito na mikutano yote k.m. Roll Calls

**(iv)** Kutunza muda wa ratiba nzima ya shule.

**(v)** Kufanya maandalio ya jioni (Preparation)

**(vi)** Kufanya majaribio na mitihani yote atakayopewa. Akiacha kufanya mtihani/jaribio atahesabiwa kutumia rasilmali za shule vibaya na hivyo atapaswa alipe "ream" moja ya karatasi kwa kila mtihani aliokosa bila sababu za msingi.



CamScanner

## 3. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Uasherati na ushoga.
(iii) Matumizi ya kilevi cha aina yeyote.
(iv) Uvutaji wa sigara,bangi au madawa mengine ya kulevya
(v) Ubakaji na ulawiti
(vi) Makosa ya jinai
(vii) Kupiga au kupigana
(viii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(ix) Kudharau Bendera ya Taifa
(x) Kuoa au kuolewa
(xi) Kumpa mimba msichana/mwanamke
(xii) Kutohudhuria vipindi vya masomo bila sababu ya msingi.
(xiii) Kukataa adhabu
(xiv) Kunyanyasa wanafunzi wengine
(xv) Kulala nje ya shule bila ruhusa maalumu
(xvi) Kuanzisha, kuhamasisha, au kushiriki mgomo na vitendo vya uvunjifu wa amani, fujo au kufanya maandamano yasiyokuwa halali/kibali.
(xvii) **Kumiliki simu ya mkononi, radio, ipad au camera**.
(xviii) Kupata ujauzito
(xix) Kutoa au kushiriki kutoa mimba

### (B) MAKOSA MENGINE.

- Hairuhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi bila ruhusa.
- Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila sare ya shule
- Hairuhusiwi kuingia katika vilabu vya pombe na baa au 'night clubs',betting points, n.k
- Hairuhusiwi kuvaa makoti makubwa, makofia (Boshori) au mitandio.
- Haituhusiwi kuvaa pete, bangili, hereni, mikufu au kidani.
- Hairuhusiwi kumpeleka mgeni yeyote bwenini au kumruhusu kulala bwenini.
- Hairuhusiwi kwenda na ndala/yeboyebo bwaloni

## 4. MABWENI:

Wanafunzi hawaruhusiwi kupika mabwenini au sehemu yoyote ile, kutumia pasi za umeme mabwenini au kuwa na 'heater'. Pia hawaruhusiwi kuunganisha umeme au kutengeneza unapokuwa na hitilafu.

## 5. MATIBABU:

i. Wagonjwa wanatakiwa kufuata ratiba iliyowekwa ya huduma ya Zahanati ya shule ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.
ii. Itokeapo dharura ya ugonjwa wakati wa masomo, itamlazimu mwanafunzi kupata kibali cha maandishi kutoka malezi ili aweze kutibiwa zahanati.
iii. Ili kuweza kutibiwa katika hospitali ya Wilaya au Mkoa, mwanafunzi anatakiwa aruhusiwe na Mganga/nesi wa shule na pia kuomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu.
iv. Kama mwanafunzi amelazwa hospitali ni lazima arudi shuleni mara tu baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini na kuripoti kwa Mkuu wa shule.
v. Shule haina utaratibu wa kuwapa wanafunzi vyakula maalumu (special or light diet) wazazi/walezi wana jukumu la kuona ni jinsi gani watoto wao wenye mahitaji maalumu ya vyakula watakavyohudumiwa kwa kuwasiliana na ofisi ya Malezi
vi. Mwanafunzi awe na **daftari dogo** kwa ajili ya matibabu katika zahanati ya shule.



CamScanner

## FOMU YA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.

JINA LA MWANAFUNZI:________________________________________

TAREHE YA KUZALIWA:________________________________________

JINA LA MZAZI/MLEZI:________________________________________

UHUSIANO:________________________________________

KAZI YA MZAZI/MLEZI:________________________________________

### KIAPO CHA UTII:

**MIMI** (Jina la mwanafunzi) ________________________________________

Nikiwa mwanafunzi wa Shule hii nakubali kuwa, Umma wa Nchi hii ya Tanzania ndiyo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia Nchi yangu kwa nguvu zangu zote na kwa uadilifu. Ninaahidi kwa kipindi chote nitakachokuwa katika shule hii nitakuwa mtiifu, sitoshiriki katika mgomo, fujo wala makosa ya jinai. Nitalinda amani na utulivu wa shule kwa njia zozote ikiwemo kutoa taarifa kwa uongozi wa shule kuhusu jambo lolote linaloashiria uvunjifu wa amani shuleni.

Ninajua kuwa serikali inatumia raslimali zake nyingi kugharamia elimu yangu na mimi ninaahidi kuwa masuala ya taaluma nitayapa kipaumbele cha kwanza ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wasio walimu, na wanafunzi wenzangu wote na kuhudhuria vipindi vyote darasani.

Nikiwa na malalamiko au maoni yeyote nitayafikisha kwa uongozi wa shule kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

**Tarehe**________________________ **Sahihi**____________________

### KIAPO CHA MZAZI/MLEZI.

Mimi mzazi/mlezi wa (jina la mwanafunzi)

______________________________________________________

Ninakiri kuwa nimesoma, nimeelewa na ninakubaliana na sheria, kanuni, na taratibu zote zilizoainishwa za kujiunga na shule hii, na pale mwanangu atakapozikiuka hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

**Sahihi**________________________ **Tarehe**____________________

**<u>FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI</u>**

**SEHEMU A:**

1. **Jina (Majina Matatu):** [ ] [ ]
2. Tarehe ya kuzaliwa
3. Utaifa [ ] Mkoa [ ]
   Wilaya [ ] Kabila [ ]

4. **Taarifa ya kubaini wanafunzi Yatima**

(i) Baba na Mama wote walikwishafariki ☐

(ii) Baba yupo, Mama alikwishafariki ☐

(iii) Mama yupo Baba alikwishafariki ☐

(iv) Baba na mama wote wapo ☐

5. Jina la Baba/Mlezi

Kazi yake Anwani ya Baba/Mlezi

Namba ya simu ya Baba/Mlezi

Anwani ya anakofanyia kazi

6. Jina la Mama/Mlezi

Kazi yake Anwani ya Mama/Mlezi

Namba ya simu ya Mama/Mlezi

Anwani ya anakofanyia kazi Je, wazazi wako wanaishi pamoja? *(Weka* ✓ panapohusika) **Ndiyo** ☐ **Hapana** ☐

7. Dini yako Dhehebu

8. Taarifa za maendeleo shuleni zitumwe kwa nani?

Jina Anwani yake

*Weka alama ya vema (✓) panapohusika.*

**TAARIFA KUHUSU SHULE ANAYOTOKA MWANAFUNZI:**

9. Jina la shule ya msingi/sekondari uliyosoma:

Jina la Mwl Mkuu/Mkuu wa Shule hiyo:

Anwani ya shule hiyo ni

Namba ya simu ya Mkuu wa shule Uliyotoka

Namba uliyofanyia mtihani (Index No



CamScanner

**ORODHA YA NDUGU/JAMAA WA MWANAFUNZI:**

Fomu hii ijazwe na kila mzazi wa mwanafunzi akitoa maelezo sahihi ya Ndugu Jamaa zake watano watakaompa mtoto wake huduma mbalimbali wakati akiwepo hapa shuleni. Watakaoorodheshwa ndio pekee watapata ridhaa ya kushughulikia masuala ya mwanafunzi awapo shuleni hususani yanapotokea matatizo ya kinidhamu.

| S/N | JINA LA NDUGU/JAMAA | MNAVYOHUSIANA | ANWANI YAKE NA NAMBA YAKE YA SIMU | PICHA (PASPORT SIZE) ZA WAZAZI/ NDUGU/JAMAA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

**NATHIBITISHA KUWA TAARIFA HII NI SAHIHI:**

Sahihi ya Mzazi/Mlezi________________________________________

Sahihi ya Mwanafunzi________________________________________

Tarehe__________________________________________________



CamScanner

**MOSHI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by a Medical Officer (Government hospital)

NAME:………………………………………………………………FORM………………………………………

BLOOD COUNT

(Red and White) ………………………………………………………………………………………………

STOOL EXAMINATION……………………………………………………………………………………

URINE ANALYSIS……………………………………………………………………………………………

STAPHILIA TEST……………………………………………………………………………………………

T.B. TEST………………………………………………………………………………………………………

EYE TEST………………………………………………………………………………………………………

EARS……………………………………………………………………………………………………………

CHEST…………………………………………………………………………………………………………

SPLEEN…………………………………………………………………………………………………………

ABDOMEN……………………………………………………………………………………………………

ADDITIONAL information e.g. Physical defects or impairments……………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

Infections; chronic or family diseases etc……………………………………………………………

Please certify that the above is fit to be enrolled at Moshi Technical Secondary School

Signature………………………………………………………………………………………………………

Designation……………………………………………………………………………………………………

Station…………………………………………………………………………………………………………

Date……………………………………………………………………………………………………………

NB.TO MEDICAL OFFICER: At the time of examination please TREAT the individual for any Ailment you note.



CS CamScanner

## SARE NA VIFAA VYA KUJIKINGA (PPE)

| Na. | SARE/KIFAA | MAELEZO | Na. | SARE/KIFAA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 |  | Sketi-Iwe ndefu hadi kwenye vifundo vya miguu | 6 |  | Miwani -Isiwe ya rangi |
| 2 |  | Suruali-Isiwe ya kubana yenye 'turn up' | 7 |  | Kofia-Iwe ngumu ya rangi ya njano |
| 3 |  | Ovaroli- liwe na mifuko mikubwa | 8 |  | Mask-Iwe inafaa kufua |
| 4 |  | Reflector-Iwe ya njano | 9 |  | Gloves -ziwe nyeusi |
| 5 |  | Safety boot-Iwe nyeusi | | | |



CamScanner